BARAZA LA MASOKO YA MITAJI

CAPITAL MARKETS TRIBUNAL

# Rafiki wa Soko

# JARIDA LA CMT

| JUZUU YA 1 | SHERIA | KANUNI | MAMLAKA |
|---|---|---|---|
| Toleo la 1 | Sheria ya CMS | Kanuni za CMST | Sawa na Mahakama Kuu |

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Kuanzishwa | 1 |
| Uongozi | 2 |
| Wigo wetu | 3 |
| Kupanua wigo wa Usimamizi | 4 |
| Mapinduzi Kidigitali | 5 |
| Uhamasishaji na Uelimishaji | 7 |
| Ulinganishaji wa Kimataifa | 11 |

# UTANGULIZI: JARIDA LA CMT (JUZUU YA 1, TOLEO NAMBA 1)

Karibu kwenye toleo la kwanza la **Jarida la Baraza la Masoko ya Mitaji (CMT) - Rafiki wa Soko.** Toleo hili la uzinduzi linatoa muhtasari wa dhamira ya Baraza la Masoko ya Mitaji (CMT) ya kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa haraka, kwa usawa na kwa utaalamu katika sekta ya fedha nchini Tanzania.



MSAJILI

MHE. DKT. MARTIN KOLIKOLI

**Mambo Muhimu katika Toleo Hili:**

- **Mamlaka Yetu:** Fahamu kuhusu mamlaka ya Baraza kama chombo huru cha kisheria chenye hadhi sawa na Mahakama Kuu, chenye jukumu la kusikiliza na kuamua migogoro na rufaa zinazohusu masoko ya mitaji, dhamana na bidhaa.
- **Mageuzi ya Kidijitali:** Uzinduzi wa Mfumo wa Usimamizi wa Mashauri (Case Management System – CMS), unaowezesha ufunguzi wa mashauri kwa njia ya mtandao (e-filing), ufuatiliaji wa mwenendo wa mashauri kwa wakati halisi, pamoja na kuongeza uwazi katika utoaji wa huduma.
- **Uhamasishaji na Kujifunza kwa Taasisi Nyingine:** Muhtasari wa kampeni zetu za uelimishaji wa umma zilizofanyika nchini kote, pamoja na ziara za kimkakati za kujifunza na kubadilishana uzoefu zilizofanyika nchini Kenya, Zambia, Kanada, Korea Kusini na Singapore.

Tunakukaribisha usome toleo hili na kujionea jinsi Baraza la Masoko ya Mitaji linavyoendelea kuimarisha imani ya wawekezaji, kulinda uadilifu wa masoko ya mitaji, na kuchangia kufanikisha malengo ya upatikanaji wa mitaji kupitia njia mbadala za ufadhili kama yalivyobainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.



# Nguzo ya Msingi katika Mfumo wa Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa nchini Tanzania.

**Baraza la Masoko ya Mitaji (CMT)** ni nguzo muhimu katika mfumo wa masoko ya mitaji, dhamana na bidhaa nchini Tanzania. Baraza hili lilianzishwa chini ya **Kifungu cha 139(1) cha Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMS Act)** kama chombo huru chenye jukumu la kuhakikisha kuwa haki katika masoko yetu inapatikana kwa **haraka, usawa na utaalamu** wa kipekee.

Moja ya sifa muhimu za Baraza ni hadhi yake ya kisheria. Kwa mujibu wa sheria, Baraza lina **mamlaka sawa na Mahakama Kuu ya Tanzania** katika kushughulikia mashauri ya madai yaliyo ndani ya wigo wake. Hali hii huhakikisha kuwa migogoro inayohusu masoko ya mitaji, dhamana na bidhaa inasikilizwa na kuamuliwa na chombo maalumu chenye utaalamu na uwezo unaohitajika.

**Mamlaka Huru**
Huru dhidi ya kuingiliwa na mamlaka ya kiutendaji katika mashauri yote ya masoko.

**Utaalamu wa Nyanja Mbalimbali**
Kwa kuunganisha utaalamu wa sheria, masoko ya mitaji.



# CMT inaongozwa na nani?

01 **MWENYEKITI**

Jaji wa Mahakama Kuu anayeteuliwa na Rais kwa kushauriana na Jaji Mkuu.

04 **WAJUMBE WA BARAZA**

Wajumbe wanne wenye utaalamu wa sheria na masoko ya mitaji, wanao-teuliwa na Waziri wa Fedha.

∞ **SEKRETARIETI**

Wakiwasaidia wajumbe hao, ni Sekretarieti inayoongozwa na Msajili. Sek-retarieti huhakikisha shughuli za kila siku za kiutawala zinaendelea kwa ufanisi, kuhifadhi kumbukumbu, na kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya kisheria ya Baraza.

# *Mamlaka* ya awali na ya rufaa

Baraza si tu chombo cha kusikiliza rufaa; bali, ni taasisi ya msingi ya kutatua aina mbalimbali za migogoro ya masoko. Majukumu yetu ya pande mbili yanajumuisha;

### UTATUZI WA MIGOGORO

**Tunasikiliza na kuamua migogoro ya masoko kati ya;**

- Mdhibiti dhidi ya Soko la Hisa au Mawakala wa Soko
- Wadau wa kati wa soko na wateja wao
- Makampuni yaliy-oorodheswa kwenye soko dhidi ya Mdhibiti au Soko.

### USIMAMIZI WA UDHIBITI

**Baraza hufanya mapitio ya maamuzi muhimu yanayofanywa na Mamlaka, yakiwemo;**

- Kukataa kutoa leseni, kusimamishwa na kufutwa kwa leseni
- Kusimamishwa kwa biashara au kuondolewa kwa dhamana kwenye orodha rasmi ya Soko la Hisa
- Ufafanuzi wa kisheria na uwazi wa udhibiti

### MAMLAKA YA KUFANYA MAPITIO YA MAAMUZI

**Rufaa inapowasilish-wa mbele ya Baraza, lina mamlaka ya;**

- Kuthibitisha maamuzi ya Mamlaka
- Kutengua au kurekebi-sha maamuzi yaliyofa-nywa
- Kurejesha mashauri kwa maelekezo maalum

*Rufaa inapowasilishwa mbele ya Baraza, lina mamlaka ya kuthibitisha, kutengua au kurekebisha maamuzi wa Mamla-ka, pia linaweza kurejesha shauri kwa ajili ya kuzingatiwa upya likiambatana na maelekezo maalum ili kuhakikisha haki inaendelea kutendeka.*

• KUPANUA WIGO WA USIMAMIZI

# Katika Soko la *Bidhaa*

Wigo wa usimamizi wa Baraza unavuka zaidi ya masoko ya mitaji na dhamana. Chini ya Sheria ya Soko la Bidhaa, tunatoa njia muhimu ya kisheria kwa wadau wa Soko la Bidhaa;


**RUFAA**

Iwapo mhusika hataridhika na maamuzi ya Soko la Bidhaa, kama hatua za kinidhamu, anaweza kukata rufaa kupitia Mamlaka na hatimaye mbele ya Baraza.

**UTOAJI LESENI**

Iwapo mhusika hataridhika na maamuzi ya Soko la Bidhaa au Mamlaka kwenye utoaji wa leseni, anaweza kuwasilisha shauri lake mbele ya Baraza.






## Mfumo wa usimamizi wa mashauri *sasa uko hewani*

Katika dhima yetu ya kuongeza ufanisi, tunajivunia kutangaza kwamba **Mfumo wa Usimamizi wa Mashauri wa CMT (CMS)** sasa umeanza kufanya kazi kikamilifu. Mfumo huu, unapatikana kupitia tovuti yetu kwenye kiungo cha **e-Rufaa**.

SASA UMEANZA KUFANYA KAZI KIKAMILIFU

# Pata haki kutoka mahali popote; bila haja ya kufika ofisini moja kwa moja.

01

### UWASILISHAJI WA MASHAURI

Wasilisha maombi, rufaa na nyaraka kutoka mahali popote, wakati wowote.

02

### UFUATILIAJI WA MUDA HALISI

Fuatilia mwenendo wa shauri lako moja kwa moja; hakuna haja ya kufika ofisini.

03

### UWAZI KAMILI

Rekodi za kidijitali zilizounganishwa huhakikisha kwamba haki inaendelea kutendeka.

*Mfumo huu ni uthibitisho wa dhima yetu ya kupunguza ucheleweshaji na kufanya upatikanaji wa haki uwe rahisi zaidi kadri inavyowezekana kwa mwekezaji wa kisasa. Katika juhudi zetu za kukuza ujumuishaji wa kifedha, tunahakikisha kwamba hatumuachi mtu yeyote nyuma.*




## Uhamasishaji na *Uelimishaji*

Tunaamini kwamba 'Rafiki wa Soko' anapaswa kuwepo na kuchukua hatua kwa wakati. Katika mwaka uliopita, tumejikita kikamilifu katika kushirikiana na wadau wetu.

| 83+ | 3+ | 5 |
|---|---|---|
| Mikutano ya moja kwa moja na wadau | Matukio makubwa ya umma yaliyohudhuriwa | Ziara za kimataifa za ulinganishaji zilizotekelezwa |

01

## MIKUTANO YA MOJA KWA MOJA NA WADAU

Timu ya Baraza ilifanya mikutano zaidi ya 83 ya moja kwa moja na wadau wa kati wa soko waliosajiliwa, wakiwemo mawakala wa hisa na washauri wa uwekezaji, makampuni yaliyoorodheshwa kwenye soko, wakaguzi na wanasheria; likifafanua mamlaka, wigo wa kisheria na taratibu za usikilizaji wa mashauri, pamoja na kusikiliza changamoto zinazowakabili washiriki mbalimbali soko.

DAR ES SALAAM








## 02

### WIKI YA HUDUMA ZA KIFEDHA

Tulifikisha huduma zetu katika viwanja vya Usagara, tukitoa elimu kwa wananchi kuhusu haki zao za kifedha na jinsi Baraza linavyoendelea kulinda uwekezaji wao.

TANGA






## 03

### MAONESHO YA 12 YA KIMATAIFA YA BIASHARA YA ZANZIBAR (ZITF)

Baraza lilishiriki katika tukio hili kubwa la kitaifa ili kuhakikisha ujumbe wa utendaji wa haki za masoko za kitaalamu unawafikia wananchi katika kila kona ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

ZANZIBAR






04

## SANAA PESA FESTIVAL (SABASABA YA SANAA)

Ushiriki wa Baraza ulilenga kuhamasisha haki katika masoko, kuhakikisha vipaji vya vijana bunifu vinawezeshwa kunufaika na fursa zilizopo ndani ya sekta ya masoko ya mitaji, dhamana na bidhaa.

DAR ES SALAAM

ULINGANISHAJI WA KIMATAIFA

# Kuleta *Viwango vya Kimataifa* Nyumbani

Ili kuendelea kuwa taasisi ya kiwango cha kimataifa, Baraza huendelea kujifunza kutoka kwa viongozi wa kimataifa. Tumehitimisha kwa mafanikio ziara za ulinganishaji wa kimataifa nchini Kenya, Zambia, Canada, Korea na Singapore. Ziara hizi zililenga;

| ZIARA ZA ULINGANISHAJI WA KIMATAIFA | MAENEO MUHIMU YA KUJIFUNZA |
|---|---|
| **Kenya** | › Mbinu Bora za Kimataifa katika Masoko ya Mitaji na Udhibiti wa Dhamana |
| **Zambia** | › Mbinu za Kina za Utatuzi wa Migogoro ya Soko la Bidhaa |
| **Canada** | › Kuunganisha teknolojia katika taratibu za kimahakama na udhibiti |
| **Korea** | › Utatuzi Mbadala wa Migogoro katika Masoko ya Mitaji na Bidhaa |
| **Singapore** | › Kuhakikisha upatikanaji rahisi wa haki kwa watu wenye mahitaji maalum |

Kwa kuzingatia na kutumia viwango hivi vya kimataifa, tunahakikisha kuwa Baraza linaendelea kuwa nguzo imara na ya kisasa kwenye sekta ya fedha nchini Tanzania.

# KENYA, ZAMBIA, CANADA, KOREA NA SINGAPORE













## *“Jukwaa Maalumu kwa Soko Maalumu.”*

Baraza linaendelea kujikita katika kutoa mazingira ya uwazi na ya kitaalamu kwa wadau wote, kuhakikisha kuwa gurudumu la haki ya kifedha linazunguka kwa usahihi na uadilifu.

# Wasiliana Nasi

S.L.P 1384, Ghorofa ya kwanza,
Jengo la Hazina Ndogo
(Posta – Mtaa wa Madaraka),
Dar es Salaam, Tanzania

**Barua Pepe: info@cmt.go.tz**

**Simu: +255 738 785 651**

CAPITAL MARKETS TRIBUNAL

*Rafiki wa Soko*

www.cmt.go.tz